

HALMASHAURI YA MANISPAA YA TABORA



TANGAZO LA ZABUNI

UTANGULIZI:

19/07/2022

1. Kwa kuzingatia **Waraka namba 16 wa Mwaka 2016 wa Waziri wa nchi, Ofisi ya Raisi TAMISEMI kuhusu Halmashauri na Mawakala wa kukusanya Mapato**, Halmashauri ya Manispaa ya Tabora imekusudia kutumia mfumo wa mawakala wa kukusanya mapato kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ili kuboresha ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri ya Manispaa Tabora.
2. Halmashauri kwa kuzingatia **Waraka namba 16 wa Mwaka 2016** hapo juu imekusudia kubinatsisha vyanzo vya mapato vifuatavyo;

LOT	AINA YA CHANZO	NAMBA YA ZABUNI
LOT 1	- Ushuru wa mazao mchanganyiko - Ushuru wa mazao ya misitu - Ushuru wa madini ya Ujenzi	LGA/124/2022/2023/NC/01
LOT 2	- Ushuru wa stendi ya mabasi	LGA/124/2022/2023/NC/01
LOT 3	- Ushuru wa maegesho ya magari	LGA/124/2022/2023/NC/01
LOT 4	- Ushuru wa vyoo	LGA/124/2022/2023/NC/01
LOT 5	- Ushuru wa masoko na vizimba	LGA/124/2022/2023/NC/01

3. Hivyo Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Tabora anawatangazia wafanyabiashara wenye Kampuni,kikund iau taasisi yenye/wenye sifa na uwezo wa kukusanya ushuru kwenye vyanzo vinavyobinafsishwa kuomba kazi ya ukusanyaji wa ushuru na Ada katika vyanzo hivyo.
4. Kwa kila chanzo cha mapato Halmashauri ya Manispaa imeweka kima cha chini cha ukusanyaji ambacho kila wakala atapaswa kufikia kwa wiki, na kwa mwezi.

SIFA ZA MWOMBAJI

1. Mwombaji awe raia wa Tanzania.
2. Mwombaji awe na Leseni ya biashara hai inayoendana na zabuni anayoiomba


- 3. Mwombaji awe na utambulisho wa mlipa kodi [TIN na.] na cheti cha kumaliza kulipa kodi [Tax Clearance certificate) na kama ni Kampuni iambatane na usajili wake
- 4. Mwombaji awe na vitendea kazi na aambatishe mpango wake wa wafanyakazi atakaowatumia katika ukusanyaji wa mapato
- 5. Mwombaji awe tayari kufanya kazi kwa mujibu wa Sheria ndogo na taratibu za Halmashauri ya Manispaa.

MASHARTI YA ZABUNI

1. Gharama za uendeshaji wa ukusanyaji wa mapato zitagharimiwa na mzabuni mwenyewe. Gharama hizo ni pamoja na (usafiri, umeme, maji, vifaa vya usafi na watumishi).
2. Mzabuni atatakiwa kuwasilisha fedha benki kila siku ya kazi baada ya kuchukua hati ya madai (Control number) kutoka Halmashauri ya Manispaa Tabora.
3. Mzabuni awe tayari kutumia mashine za kielektronic za Halmashauri ya Manispaa Tabora kukusanya ushuru na Ada, na si vinginevyo.
4. Mzabuni awe tayari kukusanya mapato yasiyopungua kima cha chini kilichowekwa na Halmashauri ya Manispaa Tabora.
5. Mwombaji atapaswa kuomba kiasi cha asilimia atakachopenda kulipwa kila mwezi baada ya kukusanya Mapato (Kiwango cha juu cha asilimia ya "Commision" itakuwa 10) na mwombaji anaruhusiwa kuomba LOT zaidi ya Moja..
6. Mwombaji atalazimika kulipa Ada ya Zabuni ya kiasi cha Shilingi 50,000 kwa lot fedha ambayo haitarudishwa endapo mzabuni atapata zabuni au kukosa zabuni.
7. Mwombaji atalazimika kufika ofisi ya manunuzi kununua kitabu cha zabuni.
8. Mwisho wa kuleta maombi ni tarehe 01/08/2022.saa 4:00 asubuhi na ufunguzi utafanyika ndani ya dakika 30 baada ya muda wa mwhisho wa kupokea zabuni.
9. Mwombaji awe na uzoefu wa kazi ya uwakala kwa muda usiopungua miaka miwili ya hivi karibuni.
10. Zabuni zitafunguliwa kwenye ukumbi wa Manispaa waombaji mnakaribishwa kushuhudia ufunguzi.
11. Maombi yote yatumwe kwa:-

Mkurugenzi wa Manispaa,
Halmashauri ya Manispaa,
Barabara ya Uwanja wa Ndege,
S.L.P 174,

TABORA



Dr. Peter M. Nyanja
MKURUGENZI MANISPAA MUNICIPAL DIRECTOR
HALMASHAURI YA MANISPAA - O. Box 174
TABORA. TABORA